# MWENGE WA UHURU WAMULIKA MKOA WA DODOMA MWAKA 2022

Mwenge wa Uhuru ni miongoni mwa tunu za Taifa la Tanganyika ulioasisiwa mwaka 1961 na Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ambaye ndiye Baba wa Taifa na wakati huo pia, ndipo nchi ya Tanganyika ilijipatia uhuru wake kutoka kwa wakoloni na kutangazwa Taifa huru. Hivyo Mwenge ni ishara ya kuwepo kwa Taifa huru la Tanganyika. Tokea hapo, mbio za Mwenge wa uhuru zilianza rasmi mwaka 1964 baada ya kufanyika kwa Mapinduzi matukufu ya Zanzibar ambayo yalipelekea kuzaliwa kwa Taifa jipya la Tanzania, yaani likiwa ni muunganiko wa nchi ya Tanganyika pamoja na visiwa vya Zanzibar.

Tangu kuanzishwa kwa mbio hizi, Mwenge wa uhuru umekuwa kichocheo kikubwa katika kuimarisha Uhuru wa nchi, umoja wa Taifa, kudumisha Amani, kulinda Muungano na kuhamasisha maendeleo ndani na nje ya Taifa la Tanzania. Kuanzia mwaka 1964 hadi mwaka 1992, mbio za Mwenge zilikuwa zikiratibiwa na kusimamiwa kitaifa na vyama vya TANU na ASP ambapo baadae vyama hivi viliungana na kuzaliwa Chama Cha Mapinduzi CCM, hivyo uratibu wa mbio hizi ulifanywa kupitia Jumuiya zake za umoja wa vijana, UVCCM.

Mwenge wa mwaka 2022 umeadhimisha miaka 30 tangu mbio za Mwenge wa uhuru zirejeshwe chini ya uratibu na usimamizi wa Serikali. Utaratibu huu ulitokana na mabadiliko ya kimfumo na kidemokrasia baada ya nchi yetu kuingia kwenye mfumo wa vyama vingi vya siasa mwaka 1992. Mabadiliko hayo yalilenga kuthibitisha kuwa, mwenge wa uhuru hauna itikadi za kisiasa, dini wala kabila bali ni mali ya watanzania wote bila kujali tofauti zao.

# MWENGE WA UHURU WAMULIKA MKOA WA DODOMA MWAKA 2022

Mbio za Mwenge wa uhuru kwa mwaka 2022 Mkoa wa Dodoma, zilianza na kupokelewa rasmi Agosti 16, 2022 katika Halmashauri ya Wilaya ya Bahi kwenye viwanja vya shule ya msingi Bahi sokoni, Kata ya Bahi ambapo ndipo makutano ya hafla ya makabidhiano yalifanyika baina ya Mikoa ya Dodoma na Singida. Hafla hiyo ilihudhuriwa na ndugu Sahili Nyanzabara Geraruma, kiongozi wa mbio za mwenge wa uhuru kitaifa kwa mwaka huu, pamoja na wakimbiza mwenge wa uhuru kitaifa katika mikoa mbalimbali waliambatana katika msafara huu wa kupokea mwenge wa Taifa ambayo ni kazi ya kizalendo.

Mwenge wa uhuru ukiwa katika Mkoa wa Dodoma, ulipita katika Wilaya zote saba (7) za Mkoa pamoja na Halmashauri zake nane(8) ambazo ni Bahi, Dodoma Jiji, Chemba, Kondoa DC, Kondoa TC, Chamwino , Mpwapwa na Kongwa. Mbio za mwenge Mkoa wa Dodoma zilikimbia umbali wa kilometa 1162 na kupitia jumla ya miradi 39. Kati ya miradi hiyo 39, 19 ilitembelewa miradi 10 iliwekewa mawe ya msingi na 10 ilizinduliwa, jumla ya thamani ya miradi yote hiyo ikiwa ni Shilingi 14,156,615,332.

Miradi hii ni sehemu ya miradi mingi ya maendeleo inayotekelezwa na Mkoa kwa sasa. Mkoa unatoa shukran za dhati kwa Rais wa Jamhuri ya muhungano wa Tanzania Mhe.Samia Suluhu Hassan kwa kusaidia fedha za miradi mingi na mikubwa ya kimkakati kwenye sekta ya Miundombinu, Ujenzi, Usafirishaji, Kilimo, Elimu, Afya, Biashara pamoja na Huduma mbalimbali.

# MWENGE WA UHURU WAMULIKA MKOA WA DODOMA MWAKA 2022

Mbio za Mwenge wa uhuru mwaka huu zimebeba ujumbe usemao, ***'SENSA NI MSINGI WA MIPANGO YA MAENDELEO, SHIRIKI KUHESABIWA, TUYAFIKIE MAENDELEO YA TAIFA'.***

## HALMASHAURI YA WILAYA YA BAHI

Halmashauri ya Wilaya ya Bahi, ulikimbia umbali wa kilometa 87, Mwenge ulikimbia na kupita eneo la sehemu Bahi sokoni, Eneo la mnadani, Mpamantwa, Kigwe, Chigongwe na Bahi makulu ambapo ulitembelea miradi mbalimbali kama vile Mradi wa uogeshaji mifugo, Mradi wa shule shikizi uliopo katika Kijiji cha Mpamantwa, Mradi wa kikundi cha vijana Technician cooperation, Mradi wa maji, Mradi wa utoaji huduma za mionzi (x-ray na utra sound) katika Hospital ya wilaya na Mradi wa ujenzi wa boksi kalavati la barabara ya Mizima.

## HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA

Katika Halmashauri ya Jiji la Dodoma Mwenge wa uhuru ulikimbia umbali wa kilometa 191.5 na kupita maeneo ya Chigongwe, njia panda ya kigwe, Shule ya sekondari Nala, Dodoma Makulu, Kisasa, Nanenane, Nzunguni, Ipagala, Shule ya msingi Mtemi Mazengo, Chan`gombe, Shule ya msingi Chan`gombe na Kijiji cha Babayu ambapo miongoni mwa miradi iliyotembelewa ni ujenzi wa shule ya msingi ya mtaala wa Kiingereza Msangalale, mradi wa ujenzi wa barabara ya kisasa (Nyumba 300\FFU – Barabara ya Morogoro, KM 1.0 ) kiwango cha lami, Mradi wa kikundi cha KIU YA UFANISI, Mradi wa Hosteli ya Southern Empire na Mradi wa ujenzi wa kituo cha Afya cha Chan`gombe.

# MWENGE WA UHURU WAMULIKA MKOA WA DODOMA MWAKA 2022

## HALMASHAURI YA WILAYA YA CHEMBA

Kwa Halmashauri ya wilaya ya Chemba, Mwenge ulikimbia umbali wa kilomita 250 katika sehemu ya vijiji vya Babayu, Hamia, Makorongo, Farkwa, Rofati, Gwandi, Chemba na Bukulu. Miradi iliyoweza kufikiwa ni pamoja na ujenzi na usambazaji wa maji kijiji cha Hamia, ujenzi wa kituo cha Afya cha Farkwa, ukarabati wa josho la mifugo la kiiji cha Rofati, Mradi wa ujenzi wa nyumba ya watumishi (3 IN 1) katika Hospitali ya wilaya ya Chemba, Taarifa ya kikundi cha Vijana cha Kimau (KIMAU YOUTH GROUP), ujenzi wa jengo la ofisi ya mkurugenzi mtendaji wa Halmashauri ya wilaya, ujenzi wa kituo cha afya cha Pahi, ujenzi wa barabara ya Mnenia –Disa kwa kiwango cha changarawe na Mradi wa vijana wa kibaoni Youth Group.

## HALMASHAURI YA WILAYA YA KONDOA DC

Ukiwa wilayani Kondoa DC Mwenge wa Uhuru ulipitia mradi wa usambazaji maji Bukulu na kuzindua mradi wa maji Bukulu, baada ya hapo ulienda eneo la mradi wa ujenzi wa jengo la Utawala la Halmashuri na kuweka jiwe la msingi la mradi huo.Baada ya hapo mwenge wa uhuru ulitembelea mradi wa kikundi cha vijana cha Kibaoni Youth Group kikundi kinachojihusisha na uzaji wa mafuta ya alizeti, baadae ulitembelea mradi wa ujenzi wa barabara ya Mnenia Itololo-Dissa Kisese na kuweka jiwe la msingi. Baada ya hapo Mwenge wa uhuru Ulitembelea na kuweka jiwe la msingi mradi wa ujenzi wa kituo cha Pahi na kugawa vyandalua kwa mama wajawazito.Wilayani Kondoa DC Mwenge wa Uhuru ulikimbizwa umbali wa Kilomita 88.6.

# MWENGE WA UHURU WAMULIKA MKOA WA DODOMA MWAKA 2022

**HALMASHAURI YA WILAYA YA KONDOA TC**

Mwenge ulipitia Miradi ya maendeleo Kondoa kama vile Mradi wa usambaaji maji, Mradi wa ujenzi wa Barabara ya Kisengo –Kingale, Msui –Kingale –Serya, Mradi wa kikundi cha vijana cha Mwangaza, ujenzi wa Shule Mpya ya Sekondari kata ya Kondoa Mjini, na ujenzi wa Kituo cha Afya cha Serya Pia mwenge ulipita sehemu kama Uwanja Wa Michezo wa Bukulu, Sekondari ya Bukulu, Jengo la Utawala Halmashauri ya Bukulu, Mradi wa ujenzi wa jengo la utawala Halmashauri, Mradi wa kikundi cha vijana kibaoni youth Group, kijiji cha Mnenia, Shule ya Sekondari ya Abeid Amani Kaume, Kituo cha Afya cha Pahi, Uwanja wa Michezo wa Shule ya msingi Busi na Shule ya msingi Busi na Bicha. Aidha mwenge ulikimbia umbali wa kilomita 250.

**HALMASHAURI YA WILAYA YA CHAMWINO**

Katika Wilaya ya Chamwino mwenge ulikimbia sehemu kama Haneti, Itiso, Dabao, Msanga, Chamwino kibarangoni, Handali, Mvumi mission na Kiegea na ulikimbia umbali a kilometa 348.5.

Miradi iliyotembelewa ni pamoja na uzinduzi wa zoezi la chanjo, uogeshaji na utambuzi wa mifugo, ujenzi wa kituo cha Afya Itiso, Mradi wa maji katika Kiiji cha Dabalo, ujenzi wa vyumba vitatu vya madarasa na ofisi moja katika Shule ya sekondari Msanga, kikundi cha vijana cha wasakatonge na ujenzi wa barabara ya kiwango cha lami Mvumi Km 1.1

# MWENGE WA UHURU WAMULIKA MKOA WA DODOMA MWAKA 2022

**HALMASHAURI YA WILAYA YA MPWAPWA**

Katika Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa, Mwenge ulikimbia umbali wa kilometa 99.2 katika maeneo ya Kiegea Ng`hambi, Mpwapwa Mjini, Ukumbi wa Mkuu wa wilaya, Ving`hawe, Kiwanja cha Mtejeta, na Kzongwa sokoni. Pia mwenge uliweza kukagua miradi ya ujenzi wa kisima cha maji cha Kiegea, Ujenzi wa Shule Mpya ya Sekondari Ng`hambi, ujenzi wa jengo la wagonjwa Mahututi (ICU) katika Hospitali ya wilaya, Ukarabati wa Barabara yenye urefu wa Km 1 kwa kiwango cha lami-Mpapwa Mjini na kikundi cha vijana Ebenee Ving`hawe.

**HALMASHAURI YA WILAYA YA KONGWA**

Kwa upande wa Hamashauri ya Wilaya ya Kongwa, Mwenge ulitembelea miradi ambayo ipo katika Halmashauri hiyo kama vile, ujenzi wa jengo la dharura (EMD) katika Hospitali ya Wilaya, kikundi cha twende pamoja wasakatonge kata ya Kongwa, ujenzi wa kituo cha Radio Zabibu Fm 105.7 MHZ kilichopo Wilayani humo na mradi wa maji kijiji cha Ijaka. Hiyo ni baadhi ya miradi ambayo Mwenge uliweza kuitembelea kupitia maeneo kama Kongwa, Shule ya sekondari St.Fransis, Kongwa mjini, Kituo cha Radio Zabibu FM, Ibwaga, Sagara, Mlali-Iyegu, Shule ya Sekondari St. Clara, Kibaigwa, Shule ya Sekondari St.Pio, uwanja wa michezo wa Shule ya Msingi Kibaigwa, Ukumbi wa St.Pio na Gairo. Mwenge ulikimbia umbali wa kilomita 99.6.

# MWENGE WA UHURU WAMULIKA MKOA WA DODOMA MWAKA 2022

**HITIMISHO**

Tunapenda kutoa shukrani za dhati Kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe Samia Suluhu Hassan kwa kuridhia mbio hizo kuendelea kila mwaka, mbio ambazo hukagua, huweka jiwe la msingi na kuzindua miradi mbalimbali katika maeneo ambako mbio hizo hupita.

Itoshe kusema kwamba baada mwenge wa Uhuru kupita katika maeneo yote ya mkoa wa Dodoma, ambapo mwenge huo ulikimbia umbali wa kilometa 1162 na kupitia jumla ya miradi 39. Kati ya miradi hiyo 39, 19 ilitembelewa miradi 10 iliwekewa mawe ya msingi na 10 ilizinduliwa yote ikiwa na thamani Shilingi 14,156,615,332. Miradi yote hiyo ilipitishwa.

Pongezi kubwa ziende kwa uongozi wa mkoa wa Dodoma, menejimenti, wakuu wa wilaya, wakurugenzi wa halmashauri pamoja na menejimenti zao kwa kufanya kazi kwa juhudi, nidhamu na maarifa hali kadhalika wananchi wa Dodoma ambao nao wamekuwa wakiienzi miradi hiyo kwa kuonyhesha ushirikiano na kuitunza.

**ASANTE.**

**MWISHO**